IFDC

# I.Habari kuhusu bidhaa

# Mada ya 26b

# Jinsi ya kutumia vifaa vya shamba

# JARIDA LA UHAKIKA

## I. Habari kuhusu bidhaa

## Mada ya 26b: Jinsi ya kutumia vifaa vya shamba

Vifaa vya shamba vinasaidia na ni muhimu sana vinapotumiwa vyema. Utumiaji usio sahihi wa vifaa hivi unaweza kusababisha majeraha kwa anayevitumia au kuharibika kwa vifaa au mimea.

### 1. Vifaa vya kutayarisha shamba/Kufyeka

| Kifaa | Jinsi ya Kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Panga** | Shika mpini kwa mkono mmoja halafu upembee ukiuelekeza upande wa chini ili kukata magugu, tete na matawi madogo. | Tumia kwa uangalifu. Bapa yaweza kusababisha majeraha makubwa. Fungia baada ya matumizi kwa sababu unaweza kutumiwa kana silaha hatari |
| **Shoka** | Weka mpini kwenye kichwa cha shoka. Shika mpini kwa mikono miwili halafu pembea ukiekeza upande wa chini ili kuchanja mbao na kukata chini miti. | Tumia kwa uangalifu. Bapa yaweza kusababisha majeraha makubwa. Fungia baada ya matumizi kwa sababu unaweza kutumiwa kana silaha hatari |
| **Sululu** | Weka mpini kwenye kichwa cha sululu. Shika mpini kwa mikono miwili halafu pembea ukielekeza upande wa chini ili kuchimba mashimo au mitaro na kukata vichaka. | Tumia kwa uangalifu. Bapa yaweza kusababisha majeraha makubwa. Fungia baada ya matumizi kwa sababu unaweza kutumiwa kana silaha hatari |
| **Sepetu** | Tumia mikono miwili kushika mpini. Tumia sepetu kulegeza udongo, kuchimba mashimo au kuchota mchanga. Tumia mguu kukikanyaga kichwa cha sepetu ili kukifinyilia udongoni | Tumia kwa uangalifu; inaweza kusababisha majeraha mabaya. Usitumie na miguu wazi |
| **Rato** | Tumia mikono miwili kushika mpini. Tumia rato kulegeza udongo. Tumia miguu kukanyaga | Tumia kwa uangalifu; inaweza kusababisha majeraha mabaya. Usitumie |

| | | |
|---|---|---|
| | kwenye kichwa ili kukifinyilia udongoni. | na miguu wazi |

## 2. Vifaa vya kuandaa udongo kwa upanzi

| Jina la kifaa | Jinsi ya kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Plau ya kuvutwa na ng'ombe** | Funga ngo'mbe na nira kwa plau. Mtu mmoja aongoze ng'ombe mbele, akivuta plau nyuma yake. Mtu mwingine ashike mikono ya plau na kuielekeza. Ulimi wa plau hukata na kufungua udongo. | Weka mbali na watoto. Linda ngo'mbe vyema kwa kuwapa maji na mapumziko wakati wa mchana |
| **Plau ya diski ya kuvutwa na wanyama** | Ni kama plau ya kuvutwa na ng'ombe | Ni kama plau ya kuvutwa na ng'ombe |
| **Kifaa cha kulima udongo cha kuvutwa na wanyama** | Ni kama plau ya kuvutwa na ng'ombe | Ni kama plau ya kuvutwa na ng'ombe |

## 3. Vifaa vya Kupanda

| Jina la kifaa | Jinsi ya kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Mashine ya kupandia inayovutwa na wanyama** | Funga ng'ombe au punda na nira kwa kifaa hicho. Mtu mmoja aongoze ng'ombe au punda mbele, akivuta mashine hiyo nyuma yake. Mtu mwingine ashike mikono ya mashine ya kupandia na kuielekeza. | Hakikisha mbegu zimeachiliwa na mashine hiyo |
| **Mashine ya kupandia (aina ya kusukumwa)** | Jaza sehemu ya ndoo ya mbegu ya mashine hiyo na mbegu. Sukuma mashine mbele ukielekeza kwa laini. | Hakikisha mbegu zimeachiliwa na mashine hiyo |
| **Kijiti cha mbegu cha kupanda** | Beba mbegu kwa mfuko ukitembea. Tengeneza shimo udongoni ukitumia kijiti na uangushe mbegu moja ndani. Funika mbegu na udongo ukitumia miguu yako. | Kuwa mwangalifu ili usitengeneze shimo refu/lililoenda chini sana |

## 4. Vifaa vya kuondoa magugu

| Jina la kifaa | Jinsi ya Kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Jembe** | Weka mpini kwenye kichwa cha jembe. Tumia mikono miwili | Tumia kwa uangalifu. Inaweza kusababisha |

| | | |
|---|---|---|
| | kupembea ukielekeza upande wa chini ili kuchimba mashimo au kutoa magugu udongoni. | majeraha mabaya isipotumiwa kwa uangalifu |
| **Jembe la kusukuma** | Shika mpini na mikono miwili. Fanya mwendo wa kupeperusha na kichwa cha jembe juu au chini tu ya sakafu ya udongo. Hukata magugu kutoka kwa mizizi. | Tumia kwa uangalifu. Inaweza kusababisha majeraha mabaya isipotumiwa kwa uangalifu |

## 5. Vifaa za Kuvuna

| Jina la kifaa | Jinsi ya Kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Mundu** | Shika kwa mkono mmoja. Kusanya ngano au mazao mengine kama hayo ukitumia mkono mwingine ili kufanya fungu. Weka bapa ya kukata ya mundu kwenye fungu na uvute kwa nguvu. Bapa itakata fungu hilo. | Tumia kwa uangalifu. Inaweza kusababisha majeraha mabaya isipotumiwa kwa uangalifu |
| **Kisu cha miwa** | Shika mkono/mpini wa kisu na ukate miwa | Tumia kwa uangalifu. Inaweza kusababisha majeraha mabaya isipotumiwa kwa uangalifu |
| **Kifaa cha kubambatua mahindi** | Toa bunzi ya mahindi ukitumia mikono kutoka kwenye mimea. Weka bunzi ya mahindi kwenye kifaa hicho halafu uzungushe mkono. Meno ya kifaa hicho itabambatua mahindi kutoka kwa bunzi. | Tumia kwa uangalifu. Inaweza kujeruhi vidole vya mkono |

## 6. Vifaa vya Kusafirisha

| Jina la kifaa | JInsi ya kutumia | Onyo |
|---|---|---|
| **Toroli** | Weka mbolea, mbegu na mizigo mingine katika mahali pa kubebea. Shika mikono yote miwili ya toroli na uinue hadi gurudumu pekee ndilo libakie sakafuni na kusukuma toroli mbele | Usiweke mizigo kupita kiasi. Inaweza kusababisha majeraha mabaya kwa mgongo wa mtu anayesukuma. |
| **Mkokoteni unaovutwa na** | Funga ng'ombe ukitumia nira kwa mkokoteni. Weka mizigo kwa | Usiweke mizigo mingi kupita kiasi. Linda mnyama vyema |

| | | |
|---|---|---|
| **ng'ombe au wanyama wengine** | mkokoteni na uongoze mnyama mbele. Mkokoteni utafuata | kwa kuupatia maji na mapumziko wakati wa mchana |
| **Kitoroli cha kuvutwa na wanyama cha kuteleza juu ya theluji** | Funga mnyama ukitumia nira kwenye toroli. Weka mizigo na uongoze mnyama mbele. Kitoroli kitafuata. Epuka maeneo yalio na mawe kwa sababu kitoroli kitakwama kwenye mawe. | Usiweke mizigo mingi kupita kiasi. Linda mnyama vyema kwa kuupatia maji na mapumziko wakati wa mchana |

# MWONGOZO

## I. Habari kuhusu bidhaa

## <u>Mada ya 26b:</u> Jinsi ya kutumia vifaa vya shamba

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi

**Muda unaohitajika:** Dakiki 45

**Maandalizi:**

☑ Karatasi ilio na kichwa: *Jinsi ya kutumia vifaa vya shamba*

☑ Vifaa vya shamba au picha zavifaa hivyo kutoka 30a

☑ Kadi za rangi zilizo na vifaa vya shamba vifuatavyo (kutoka kipindi cha 26a):

- *Panga*
- *Shoka*
- *Sululu*
- *Sepetu*
- *Plau ya kuvutwa na ng'ombe*
- *Kijiti cha mbegu cha kupanda*
- *Jembe*
- *Mundu*
- *Mkokoteni unaovutwa na ng'ombe*
- *Kitoroli cha kuvutwa na wanyama cha kuteleza juu ya theluji*

# Mwanzo

**U**sikivu: Weka vifaa vya shamba mbele yako na uwakumbushe washiriki kwamba tumeangazia vifaa tofauti vya shamba katika kipindi kilichopita.

**K**ichwa: Waambie washiriki kichwa huku ukiwaonyesha karatasi ilio na kichwa: *Jinsi ya kutumia vifaa vya shamba*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika kutumia vifaa vya shamba

**M**alengo: Kueleza jinsi ya kutumia vifaa vya shamba.

**M**anufaa: Ukiuzia wakulima vifaa hivi, unafaa uwe na uwezo wa kuwashauri wakulima jinsi ya kuvitumia. Kuwapa wateja habari hii kutahakikisha wanarejea kununua bidhaa kutoka kwa duka lako.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, tutaangazia tu vifaa vinavyotumika kila mara. Kutakuwa na habari za ziada pia katika makala watakaopewa washiriki.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Gawanya washiriki katika vikundi kumi. Patia kila kikundi kifaa cha shamba kimoja au picha ya kifaa, pamoja na kadi ya rangi ilio na jina la kifaa hicho. Kila kikundi kijadili **jinsi ya kutumia** kifaa hicho na kujadili tena **onyo** katika matumizi ya kifaa

hicho. Baada ya majadiliano, kila kikundi **kionyeshe** jinsi ya kutumia kifaa hicho kwa washiriki wengine. Kubali muda wa majadiliano.

2. Anza **maonyesho**. Kwa kila onyesho, bandika kadi ya rangi ilio na jina la kifaa pamoja na picha ya kifaa hicho ukutani na halafu kikundi kionyeshe jinsi ya kutumia kifaa hicho. Uliza maoni na hoja zaidi kutoka kwa washiriki. Toa muhtasari wa maonyesho yaliofanywa na washiriki na uongeze mawazo yako. Uliza kikundi kilicho onyesha jinsi ya kutumia kifaa hicho kama kuna onyo lolote maalumu. Kariri onyo na uongeze mawazo kama inafaa.
3. Wacha kila kikundi kionyeshe jinsi ya kutumia kifaa chake.

# Malizia

**M**uhtasari: Toa muhtasari ukirudia jinsi ya kutumia kila kifaa ambacho washiriki walionyesha jinsi ya kukitumia.

**M**aswali: Uliza washiriki umuhimu wa kutumia vifaa kwa njia inayostahili. Waulize ni kwa nini ni muhimu kwa wauza pembejeo za kilimo kushiriki habari hii na wateja wao wakulima. Uliza maagizo ya matumizi ya mbili au tatu kati ya vifaa vya shamba.

**H**atua fuatilizi: Waambie washiriki kwamba wakati ujao, mteja anapokuja kwa duka lao kununua vifaa vya shamba, wanafaa wampatie habari kuhusu jinsi ya kutumia vifaa hivyo ili apate manufaa ya juu sana kutoka kwa vifaa hivyo.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.